



# Growing up **2030** in a digital world

GOVERNING HEALTH FUTURES  
THE LANCET & FINANCIAL TIMES COMMISSION

## Kuhusu *Lancet* & Tume ya Financial Times

Wanatumia kutoka sekta, utaalamu, na malezi mbalimbali wanachangia mwongozo wao, ujuzi wao, na mawazo yao kwenye ripoti kuhusu *Kudhibiti hatima za afya 2030: Kukua katika ulimwengu wa kidijitali* (GHFutures2030). Ripoti hii itachapishwa kwenye *Lancet* mwaka wa 2021 na itaangazia kuunganishwa kwa afya ya kidijitali, akili tarakilishi (AI), na teknolojia nyingine zilizo kwenye mstari wa mbele na bima ya afya kwa wote (UHC) ili kutegemeza kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ya tatu, kwa kuzingatia hasa watoto na vijana leo, na vizazi vijavyo vya kesho.

### Jifunze zaidi:

[www.governinghealthfutures2030.org](http://www.governinghealthfutures2030.org)


## GHFutures2030 MTANDAO WA VIJANA



Teknolojia za kidijitali na data zinabadilisha mwonekano wa afya ulimwenguni na kukua leo—katika ulimwengu wa kidijitali—ni tofauti sana na ilivyokuwa miaka ishirini, kumi na hata mitano iliyopita. Kuliko wakati mwingine, COVID-19 imeweka wazi kwamba vijana wameathiriwa pakubwa zaidi na mwongezeko wa mabadiliko ya kidijitali, na kwamba wao ni mawakala wakuu wa mabadiliko katika majadiliano ya ulimwenguni pote na ya maeneo ya kwetu kuhusu kudhibiti hatima ya afya.

Katika mwaka wa 2021, *Lancet* & Tume ya Financial Times *Kudhibiti hatima ya afya 2030: Kukua katika ulimwengu wa kidijitali* ilianzisha Mtandao wa Vijana GHFutures2030 kama jukwaa la kufanyiza pamoja na kuongoza pamoja utafiti wa wakati ujao, utetezi, na kusambazwa kwa ripoti.

Mtandao huu utaleta pamoja vijana chini ya umri wa miaka 30 waliowekeza katika afya na ustawi wa vijana na hatima ya kudhibiti afya inayoundwa leo. Malengo ya Mtandao huo ni kujenga harakati iliyotengewa kudhibiti afya ya kidijitali ikichochea na mahitaji ya watoto na vijana, kuanzisha mazungumzo, matukio, na hatua zinazobuniwa na kusimamiwa pamoja na kwa ajili ya vijana na pamoja na vijana.





## Timu ya Vijana

Timu ya Vijana ya Karani wa Tume ilibuniwa mwaka wa 2020 ili kuongeza kazi ya Tume na kuhusisha vijana moja kwa moja katika matendo na mazungumzo ili kudhibiti hatima za afya.

## Timu ya Vijana inalenga:

- Kuendesha mchakato wa majadiliano kati ya Wanatume na vijana katika kiwango cha ulimwenguni, kikanda, na nyumbani ili kuhakikisha hatua na umiliki wa mapendekezo ya ripoti unaohusisha vizazi vyote
- Kupanga utafiti na mazungumzo ya wakati ujao kuhusu kudhibiti hatima za afya
- Kuzingatia nyanja za ripoti ya Tume zinazovutia kihususa vijana.

## Jinsi ya kujiunga

Tunalenga kuwa na mtandao mpana na wenye utaalamu tofauti-tofauti kama vijana tunaowawakilisha ulimwenguni pote, hivyo kuchochea ushirikiano wa maeneo na sekta mbalimbali.

Ili kujiunga, tafadhali jaza [fomu hii fupi ya dakika moja ya google](#).

Kwa maswali zaidi, tafadhali wasiliana na [youth.ghfutures2030@graduateinstitute.ch](mailto:youth.ghfutures2030@graduateinstitute.ch).

## MALENGO MAKUU

Mtandao wa Vijana GHFutures2030:

- **Utafanya kazi na vijana** katika maeneo ya jiografia na utaalamu wote ili kutetea kuhusishwa zaidi kwa vijana katika kubuni na kutekelezwa kwa sera na programu zinazohusiana na afya, teknolojia, na data
- **Utategemeza utetezi na usambazaji** wa matokeo ya Tume, ikichochea na maadili yaleyale ya kuhusisha wote, demokrasia, mshikamano, usawa, na haki za kibinadamu
- **Utawafanya wanaofanya maamuzi wawajibike** kwa kujitolea kwao kwa afya na matumizi sawa na yenye kuwajibika ya teknolojia na data
- **Utashirikiana** na mitandao mingine inayohusika katika kubadilisha sera ili kuendeleza na kudhibiti hatima za afya
- **Utaongeza sauti za vijana** na kuongoza washiriki wa mtandao huu kubuni na kuongoza pamoja utafiti wa wakati ujao, utetezi, na usambazaji wa shughuli zinazohusiana na kudhibiti hatima za afya katika ulimwengu wa kidijitali.

